NOA BONGO, JENGA MAISHA YAKO

# "KABUMBU AFRIKA - NI ZAIDI YA MCHEZO!"

## EPISODE THREE: "Mpira wa chuichui"

**MWANDISHI: Chrispin Mwakideu**

**WAHARIRI: Andrea Schmidt, Thelma Mwadazaya**

- **ORODHA YA WAHUSIKA KIPINDI CHA TATU**
- MSIMULIZI

**SCENE ONE: MEETING AT THE VIP LOBBY**

- Jonathan (mume,15)
- Mhe. Makemba (mume, 55)
- Metogba (mume, 28)

**SCENE TWO: AT THE HOTEL**

- Chedede (mume,14)
- Komora (mume,14)

**SCENE THREE: METOGBA ‘S PRESSCONFERENCE AT THE HOTEL**

- Mwanahabari na michezo (mke, 25)/
- Metogba (mume, 28)

**SCENE FOUR: AT THE PLAYGROUND**

- Chedede (mume,14)

**INTRO**

1. **NARRATOR**: Nawasalimu nyote tena, na karibuni sana katika kipindi mukipendacho,tunapopata fursa ya kunoa bongo,ili tujenge maisha yetu.Umeifungua redio yako wakati sawa kabisa wa kusikiliza makala yanayoendelea ya Soka "**Kabumbu afrika-ni zaidi ya mchezo**!".Wiki iliyopita, ndoto ya Safina ya kucheza soka ilitetereka baada ya shangazi yake kumkataza kucheza mpira. Kwengineko mambo yanazidi kupamba moto, baada ya Mheshimiwa Makemba, kutaka kukutana ana kwa ana na mkufunzi huyu wa kliniki ya soka, jee ni nani, na wataelewana kweli? Na jee, Chedede atapata fursa ya kuhudhuria hiyo kliniki ukizingatia kuwa yeye ni chokoraa? Ufafanuzi ni katika makala ya tatu, "**Mpira wa chuichui".** Kisa chetu kinaanzia na Mheshimiwa Makemba pamoja na mwanawe wanaomsubiri mcheza soka maarufu na mashuhuri barani Afrika anayecheza kwenye timu za Ulaya. Usiondoke!

**SCENE ONE: MEETING AT THE VIP LOUNGE IN A HOTEL**

2. **MHE. MAKEMBA:** Habari kaka... ah, ngoja kwanza**… (not believing his eyes)** siamini macho yangu, Metogba ni wewe! Nimefurahi sana kukutana na wewe!

3. **METOGBA:** Bila shaka wewe ndiye mgeni wangu, kwa jina naitwa Metogba... naona tayari unanifahamu, sijui unaitwa nani mwenzangu?

4. **MHE. MAKEMBA:** Makemba, Mheshimiwa Makemba. Mbunge wa Tambarare. Nimefurahi sana kufahamiana nawe. Sikutarajia kuwa shirikisho la soka nchini litamualika mtu wa hadhi yako... kabla sijasahau, huyu hapa ni mwanangu Jonathan.

5. **JONATHAN: (in shock at seeing Metogba so near)** Hu..uu..jambo

6. **METOGBA:** Sijambo Jonathan. Naam Bwana Makemba, unataka nikusaidieje? Kama unavyojua, kuna mengi ya kufanya kabla ya kliniki ya soka kuanza shughuli zake, na muda nao ni mchache... ila yote kheri. La msingi ni kuimarisha amani na maridhiano katika nchi yenu.

7. **MHE. MAKEMBA:** Kweli nakubaliana na wewe, sitochukuwa muda wako mwingi... kijana wangu Jonathan ni shabiki wako mkubwa, na mimi pia **(chuckles nervously)** nafahamu kwamba timu ya wachezaji chipukizi utakayoiteua itashiriki kwenye mechi za kirafiki barani Ulaya.

8. **METOGBA:** Ni kweli kabisa.

9. **HON.MAKEMBA:** Sasa pendekezo langu ni kuwa umuorodheshe Jonathan kwenye kikosi hicho. Yeye ni mchezaji hodari sana na angependa kufanikiwa katika soka kama vile wewe.

10. **METOGBA:** Kwa hiyo kama sikukosea, unataka nimuorodheshe kijana wako hata kabla ya kliniki kuanza mazoezi sivyo?

11. **MHE. MAKEMBA: (chuckles again)** Aha... mpe nafasi kijana wangu... na wewe hutoachwa mikono mitupu.

12. **METOGBA:** Nasikitika mheshimiwa, siwezi kufanya hivyo, kabumbu ni mchezo unaozingatia usawa bila mapendeleo... Mruhusu kijana wako aje kwenye mazoezi ya kliniki ya soka na kama atafanikiwa bila shaka nitamsajili. Kuhusu fedha, nataka ujuwe kuwa mimi na timu yangu tunayagharamia mahitaji ya wachezaji wote chipukizi 11 watakapokuwa barani Ulaya. Ikiwa kweli unataka kutoa usaidizi, tafadhali changia katika mfuko wa timu yetu. Asante na uwe na jioni njema.

13. **SFX: CHAIR BEING PULLED AS WHEN PEOPLE STAND TO LEAVE**

14. **MHE. MAKEMBA:** Subiri, hatuwezi kuyazungumzia haya huku tukipata kinywaji?

15. **METOGBA:** Mheshimiwa, umesahau kitu kimoja: Mimi ni mcheza kandanda sio mwanasiasa.

16. **NARRATOR:** Mheshimiwa Makemba hakuyatarajia majibu ya aina hiyo. Yeye amezoea kukipata kila anachokitaka kutumia mbinu yoyote ile. Jee hicho ni kikwazo? Kwa upande mwengine kwenye mkahawa pale barabarani Komora na Chedede walikuwa wanahitimisha mazungumzo yao. Tuwasikilize.

**SCENE TWO: AT THE HOTEL**

**17. SFX: VOICES OF PEOPLE TALKING, ORDERING MEALS ETC.**

**18. CHEDEDE:** Kwa hivyo, Komora, nieleze, waonaje wewe? Tujaribu bahati yetu? Tangazo lilisema vijana wote kati ya umri wa miaka 12 hadi 16 wanaruhusiwa kujiunga na kliniki hiyo ya mpira. Mimi nina miaka 14, na wewe?

**19. KOMORA: (Bursts out laughing)** Dede, kumbe kichwa chako kina matatatizo. Jitazame, tutazamane! Ni nani atakayeturuhusu kushiriki kwenye kliniki hiyo? Na hata wakitukubali, pindi watakapojua asili yako, bila shaka watakutimua, mara moja!.

**20. CHEDEDE:** Mimi sikubaliani na wewe Komora, kwani kabila langu na kabumbu ni wapi kwa wapi, eh? Mimi nacheza kwa mguu, si mdomo.

**21. KOMORA:** Basi kamueleze hayo mkufunzi wa timu ya taifa, kwani wachezaji wote wa kitaifa ni wa kabila lake... yote hayo ni kazi bure... sisi majaliwa yetu ni mitaani... upende usipende, tutaishia humu mapipani, tutakufa mumu humu mapipani.

**22. CHEDEDE:** Lakini, Komora, hii kliniki itasimamiwa na mkufunzi ambaye ni raia wa kigeni. Hatoyajali makabila yetu au ikiwa sisi ni watoto wa mitaani.

23. **KOMORA:** Kwani wewe u mgeni hapa Tambarare? Sote twajua kuwa tayari washawateuwa wachezaji wa timu hiyo na orodha imekamilika… haya ya mazoezi ya kliniki ya soka ni ya kufunga watu macho tu. Ndio mimi ni Chokoraa, lakini si mjinga.

24. **CHEDEDE: (takes a deep resigned breath)** Pengine unalolisema ni kweli... hatuna nafasi… Hii ni moja ya ndoto zangu ambayo hazitatimia kama ile ya kuwatafuta wazazi wangu halisi… **(almost in tears**) Nimesalimu amri... sitafanikiwa.

25. **KOMORA:** Usife moyo Dede, mimi na wewe tuko pamoja kama ndugu, jipe moyo. Mbona unaondoka tena?

26. **CHEDEDE:** Sijui niendako, nimefikia ukingoni.

27. **KOMORA:** Umesahau kitu basi... mpira wako huu... shika!

28. **SFX: BALL OF PLASTIC BAGS BEING CAUGHT IN BETWEEN HANDS.**

**29. NARRATOR:** Chedede aliunyaka mpira wake,cna akatokomea kwenye vichochoro vya mji wa Tambarare akiwa mnyonge na amevunjwa moyo na kauli za Komora... Je, msikilizaji,unadhani angeupuuza ushauri wa Komora?Jimbi la kwanza lilipowika tu, Chedede aliuchukua mpira wake na akaelekea kwenye kiwanja kidogo chenye vumbi ambako anacheza mpira kwa kawaida.Hakujua kuwa kitendo kile ndicho kitakachombadilishia maisha yake kabisa!Lakini kwanza tujiunge na waandishi wa habari wa michezo wanaomsubiri Metogba.

**SCENE THREE: METOGBA'S PRESS CONFERENCE**

**30. MWANAHABARI:** Ndiye yule amewasili!

**31. SFX: HUGE APPLAUSE FOLLOWED BY SOUNDS OF CAMERA FLASHES**

**32. METOGBA:** Hamjamboni mabibi na mabwana, tuanze na maswali moja kwa moja,ikiwezakana tafadhali.

**33. MWANAHABARI:** Metogba, vipi kandanda inaweza kuchangia katika harakati za kudumisha amani na maridhiano hapa nchini? Lipi lengo hasa la kliniki hii ya mazoezi?

**34. METOGBA:** Sawa, hmm… naomba nipewe mpira tafadhali... huu mpira una rangi zipi?

**35. MWANAHABARI:** Nyeusi na nyeupe..

**36. METOGBA:** Sawa! Tuchukulie rangi hizi mbili tofauti ni kama makabila mawili ya humu nchini, utaona ya kwamba rangi hizi ni sawa. Hazina malumbano, badala yake zina amani hata mpira unapotolewa pumzi... tazama...

**37. SFX: BALL BEING DEFLATED OF AIR INSIDE**

**38. METOGBA:** …Mpira wote unatoka pumzi, si upande wa rangi nyeusi tu, wala rangi nyeupe. Mpira wote. na tunapoujaza pumzi? Naiomba pampo tafadhali…

**39. SFX: BALL BEING PUMPED WITH AIR GRADUALLY**

**40. METOGBA:** Mpira wote tena umejaa kwa wakati mmoja… Sasa umuhimu wa kliniki hii ni kuunga mkono hatua za kudumisha umoja humu nchini kadhalika kuwatafuta wachezaji chipukizi wa soka ambao wanaweza kufanikiwa katika fani hii.

**41. MWANAHABARI:** Kuna tetesi na taarifa zinazoeleza kuwa tayari timu hiyo imeshateuliwa na shirikisho la kandanda. Unasemaje kuhusu hilo?

42. **METOGBA:** Kama ulivyosema hizo ni tetesi na hazina misingi yoyote**.** Ufisadi, rushwa na upendeleo wa kindugu vimeiathiri soka barani Afrika. Ila ningependa kuwahakikishia mashabiki wote wa kandanda nchini humu kuwa kila mchezaji ataheshimiwa, kutakuwa na usawa na hakuna atakayeshushwa hadhi kwasababu naelewa vizuri suala la ubaguzi kwasababu ya rangi ya ngozi yako,asili,nafasi katika jamii, tofauti za kidini au hata jinsia.

43. **MWANAHABARI:** Upi mtazamo wako kuhusu mivutano kwenye soka kati ya serikali na mashirikisho ya kandanda katika mataifa mengine barani Afrika?

44. **METOGBA:** Binafsi, naamini soka inapaswa kusimamiwa na wachezaji na sio wanasiasa. Sote tunafahamu kuwa wanasiasa wetu wanayapa umuhimu zaidi mahitaji yao. Kamwe hawayajali maslahi ya wachezaji.

45. **SFX: APPLAUSE**

46. **METOGBA:** Kabumbu ni mchezo unaowapa wachezaji wake pato kubwa zaidi kote ulimwenguni, na ukisimamiwa vizuri pato hilo litainufaisha nchi pia. Haki ya kuwa muandalizi wa kuwania vinyang'anyiro muhimu kama Kombe la Afrika au Dunia ni njia moja ya wachezaji pamoja na taifa zima kwa jumla kuiimarisha miundo mbinu na kutengeza ajira.

47. **SFX: CROWD MURMURS AND SHOUTS…MORE CAMERAS FLASHING**

48. **MWANAHABARI: (Calls out)** Metogba!Naweza kupata kumbukumbu yako kwa kutia saini kwenye fulana yangu?

49. **NARRATOR:** Pindi mkutano na waandishi wa habari ulipokamilika, Metogba aliondoka hotelini, Chedede naye alikuwa amesimama peke yake kwenye uwanja akiwa ameushika mpira wake kuukuu**.**

50. **<u>SCENE FOUR :AT THE PLAYGROUND</u>**

51. **CHEDEDE: (Speaking to himself)** Ngoja niitathmini nguvu ya mkiki wangu. mpira chini... alafu hatua kumi nyuma.

52. **SFX: FOOTSTEPS ON GRAVEL GROUND AS CHEDEDE COUNTS**

53. **CHEDEDE:** Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa, kumi, labda niongeze moja tena, kumi na moja. Sasa acha tuone kama utazuia hii penalti.

54. **SFX: BALL (OF PLASTIC) IS KICKED HARD… THEN FOLLOWED BY GLASS WINDOW BEING SHATTERED.**

55. **CHEDEDE:** Mungu wangu... nimefanya nini mimi sasa!?

**56. NARRATOR:** Kioo kile kilipokuwa kikivunjika vipande vidogo vidogo, Chedede naye alilifahamu moja. Ndoto yake pia ilikua imevunjika kwa mtindo huohuo. Lakini ni kweli?Jee amelivunja dirisha la gari la nani? Itakuwaje? Metogba naye anasubiriwa na changamoto zipi anapojaribu kuunda timu yake? Yote haya na mengine mengi yanakusubiri wewe katika kipindi kijacho. Ukipenda kusikiliza tena kipindi hiki au chengine kilichopita tembelea kurasa za tovuti zetu www.dw world.de/lbe. Mpaka wakati huo, kwa heri!